**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA MKUU WA MKOA WA DAR ES SALAAM**

# HOTUBA YA MHE. AMOS MAKALA, MKUU WA MKOA WA DAR ES SALAAM, KATIKA UFUNGUZI WA MKUTANO WA WADAU KUJADILI MAPITIO YA NAULI ZA TEKSI MTANDAO

**Tarehe:** 11 Oktoba 2022

**Mahala:** Ukumbi wa Mikutano wa Arnaoutoglou, Dar es Salaam

---

**Ndugu Mkurugenzi Mkuu wa LATRA;**

**Ndugu Wakuu wa Taasisi, Viongozi wa Serikali na Sekta Binafsi,**

**Ndugu Kaimu Katibu Mtendaji wa LATRA CCC;**

**Ndugu Wamiliki wa Vyombo vya Usafiri wa Umma;**

**Ndugu Madereva wa Teksi Mtandao;**

**Ndugu Wasafirishaji na Watoa Huduma ya Usafiri wa Umma;**

**Ndugu Wanahabari;**

**Ndugu Waandaaji wa Kikao Hiki na Wenyeji wetu;**

**Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana, Itifaki Imezingatiwa.**

**Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**

Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema kwa kuendelea kutupa uhai na kutuwezesha kukutana hapa leo tukiwa wazima wa afya, watulivu na salama katika Mkoa wetu wa Dar es Salaam. Nataka kuwahakikishia kwamba Mkoa wetu wa Dar es Salaam uko shwari, shughuli zote za kijamii, kibiashara na utoaji wa huduma mbalimbali zinaendelea kutolewa kwa amani na utulivu mkubwa. Karibuni sana Dar es Salaam.

Natambua kwamba Mkutano huu wa wadau, umetokana na maombi ya watoa huduma wa teksi mtandao (Bolt na Uber) ambao nimeambiwa viongozi wao wa Afrika Mashariki na Afrika kwa ujumla wanahudhuria kikao hiki. Napenda nichukue fursa hii kuwakaribisha sana wageni hao hapa Dar es Salaam na Tanzania kwa ujumla. Napenda kuwahakikishia kwamba, Serikali ya Awamu ya Sita, chini ya uongozi mahiri wa Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni sikivu sana na ndio maana baada ya kuwasilisha maombi yao LATRA ya kutaka kusikilizwa, fursa hiyo imetolewa kwa uwazi na bila kizuizi.

**Ndugu Mkurugenzi Mkuu na Wadau wote,**

Kwa nafasi yangu kama Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, napenda nitumie fursa hii kuipongeza sana Serikali yetu ya Awamu ya Sita kwa jitihada kubwa za kuboresha Sekta ya Uchukuzi ikiwepo miundombinu kama barabara na reli, vyombo vya usafiri

(meli/boti, mabasi ya masafa  kwenda mikoani na nchi jirani, teksi mtandao na hata kuruhusu bodaboda kuwa usafiri wa umma). Nchi yetu ina mtandao mkubwa sana wa barabara za lami, miji imepangika vizuri na sasa kuna uwekezaji mkubwa (mega project) unaoendelea wa usafiri wa reli kupitia Shirika la Reli Tanzania (TRC). Juhudi hizi za Serikali yetu zinachochea ukuaji wa shughuli za kiuchumi na kuongeza ajira na vipato kwa wananchi.

Aidha, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru waandaaji wa Mkutano wa Wadau wa Teksi Mtandao kwa kunipa heshima ya kuwa Mgeni Rasmi katika ufunguzi wa Mkutano huu muhimu wa wadau unaolenga kupokea maoni ya wadau kuhusu kufanya mapitio ya nauli za teksi mtandao. Kama alivyoeleza Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, kazi hii inafanyika kutokana na LATRA kupokea maombi ya Bolt na Uber ya kufanya mapitio ya nauli za teksi mtandao nchini kwa kuzingatia gharama za utoaji huduma kwa upande wa wamiliki wa mifumo ya teksi mtandao, madereva au wamiliki wa magari yanayotoa huduma hii, na uwezo wa abiria wa teksi kuweza kutumia huduma hii katika Mkoa wa Dar es Salaam na Tanzania kwa ujumla.

**Ndugu Mkurugenzi Mkuu na Wadau wote,**

Sote ni mashahidi kuwa Serikali ya Awamu ya Sita, chini ya Uongozi wa Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania ina nia ya dhati katika kuwezesha mazingira rafiki ya kibiashara kwa sekta binafsi hapa nchini. Haya amekuwa akiyasisitiza sana Mhe. Rais mwenyewe kwa kauli zake mbalimbali lakini pia yapo kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM), Mipango mbalimbali ya Serikali, Mipango na Makubaliano ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Nchi za SADC na hata Makubaliano ya Kikanda (Tripartite Agreements). Serikali yetu inatambua kuwa sekta binafsi ina mchango mkubwa sana katika kuchangia pato la Taifa letu kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na kulipa kodi stahiki. Aidha, sekta binafsi ina nafasi kubwa katika kutoa ajira kwa watanzania wengi zaidi kuliko ajira za Serikali yenyewe na Taasisi zake.

Nimeona niseme haya kwa kuwa ninafahamu baadhi yetu tumeajiriwa au tumejiajiri katika huduma hizi za teksi mtandao, hivyo, huduma hizi zikienda vizuri basi nasi mambo yetu pia yataenda vizuri. Na kinyume chake, huduma hizi zikienda vibaya na mambo yetu yatakuwa magumu. Kama tunavyojua, Serikali ya Awamu ya Sita imejipambanua kwa kuboresha uwekezaji ambao pia unasaidia kuongeza mzunguko wa fedha na kuongeza vipato ili kila mtanzania na wawekezaji wanufaike na uwekezaji huo.

**Ndugu Mkurugenzi Mkuu na Wadau wote,**

Usafiri wa magari ya kukodi ni muhimu sana katika kuongeza wigo wa huduma za usafiri kwa abiria hususan mijini, ili kuwezesha shughuli za kiuchumi kufanyika kwa wakati na kuboresha maisha ya Watanzania. Maboresho katika udhibiti wa huduma hii, ukiwemo udhibiti wa nauli kwa kutumia vifaa maalum vya kielektroniki yanaendana na ikiwa ni utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Usafirishaji ya Mwaka 2003, yaani *National Transport Policy 2003.* Sera hiyo imehimiza matumizi ya teknolojia sahihi katika kuboresha na kudhibiti huduma za usafiri. Hivyo, napenda kuwapongeza wabunifu na wawekezaji wote ambao wametengeneza mifumo mbalimbali ya TEHAMA inayowezesha kusimamia huduma za usafiri wa teksi mtandao na hivyo kurahisisha upatikanaji wa huduma hii. Katika hatua hii, LATRA inapaswa kuongeza usimamizi wa utendaji wa mifumo hii kwa kuzingatia Sheria na Kanuni zilizopo, kwa kujali maslahi mapana ya watumia huduma, wawekezaji na wananchi wote kwa ujumla.

**Ndugu Mkurugenzi Mkuu na Wadau wote,**

Moja ya misingi ya utawala bora ni ushirikishwaji, nasi kama wadau kwa upande wa Serikali tumefurahi kushuhudia ushiriki wenu katika Mkutano huu muhimu wa kutoa maoni yenu ili kuipa LATRA taarifa zitakazoisaidia kufanya maamuzi. Hivyo, kwa kuwa jukumu tunalofanya leo ni kupokea mapendekezo, kuyajadili na kutoa

maoni, nawasihi kila mmoja wetu, kwa kuzingatia wajibu wake, kutoa maoni yake kwa uhuru na kwa lugha yenye staha. Natoa rai kwenu wadau kuitumia vizuri nafasi hii, ili kuwawezesha wataalamu wetu kufanya kazi yao kwa ufanisi.

**Ndugu Mkurugenzi Mkuu na Wadau wote,**

Kabla sijamaliza hotuba yangu, naomba niwakumbushe LATRA, Wamiliki wa Mabasi yaendayo Mikoani na pia Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, kuhakikisha huduma za usafiri wa mabasi hayo unaoanzia Dar es Salaam, ambapo ni mabasi mengi kuliko sehemu nyingine yoyote Tanzania, inawatolewa kwa ubora unaostahiki na kwa nauli halali zilizoidhinishwa. Eneo hili tayari kuna utaratibu wa matumizi ya tiketi mtandao au tiketi za kielektroniki kuanzia tarehe 1 Septemba 2022 kwa nchi nzima.

**Ndugu Mkurugenzi Mkuu na Wadau wote,**

Baada ya kusema haya, napenda kutamka rasmi sasa kuwa **Mkutano wa Kupokea Maoni ya Wadau hapa Dar es Salaam wa Mapitio ya Nauli za Teksi Mtandao umefunguliwa Rasmi.**

Asanteni kwa kunisikiliza

**Amos Makala**

**MKUU WA MKOA - DAR ES SALAAM**

**11 OKTOBA, 2022**